

Twende Wapi?

Katiba na Afya



Kitabu hiki kimetolewa na **Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)** ikishirikiana na **Twaweza**.

Waandishi: Anna Henga, Evarist Kamwaga na Al-Amin Kheraj

Wahariri: Helen Kijo - Bisimba, Rakesh Rajani na Risha Chande

Mchoraji: Marco Tibasima

Anuanī:

SLP 75254, Dar es Salaam.

Simu: 2773048/ 2773038

Nukushi: 2773037

Barua pepe: lhrc@humanrights.or.tz

Tovuti: www.humanrights.or.tz

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakili na kutuma nakala mbili kwa LHRC.



Utangulizi

Msomaji,

Wengi tumekua tukisoma au kusikia Katiba. Zaidi ya hayo, wengi tukadhani neno au dhana hii haituhusu bali ni maalumu kwa wanasheria au wasomi tu. Ukweli ni kwamba, Katiba ni kitu muhimu mno. Kama msingi ulivyo na umuhimu katika ujenzi wa nyumba, kadhalika na Katiba ni muhimu sana kwa Taifa na watu wake. Pia ina uhusiano wa moja kwa moja na maisha yetu ya kila siku.

Kijitabu hiki kitakuwezesha kutambua maana na umuhimu wa Katiba yaani jinsi inavyogusa maisha yako. Pia kinatoa mfano wa matukio kuhusu baadhi ya harakati za wananchi waliojitelea kuzilinda haki zao za kikatiba.

Ni mategemeo yetu kuwa msomaji licha tu ya kuburudika, utajifunza na kuishi kwa mujibu wa miongozo ya Kikatiba. Zaidi ya hayo, utawashirikisha na wengine elimu uliyopata katika kijitabu hiki.

Dr. Helen Kijo Bisimba
Mkurugenzi Mtendaji - LHRC

Wahusika



Bibi - Bibi yake Bonge



Bonge - Mjukuu wa Bibi



Mpoki - Dereva bodaboda



Rehema - Rafiki yake Bonge,
Nesi Hospitali ya Wilaya

PPU!


Msimamishe
huyoooooo!

NAKUFAAA!
KAUA!

VROOOOM!

Wee
simamaaaa!

Tukaone nani
kaumizwa.




Hatuwezi
kumtibu, hakuna
dawa au vifaa.
Nitazuia tu damu
isiendelee kuvuja.

Hakuna dawa?
Kwanini?





Safari ya mjini.



Gharama ya
msafara wa magari
19 isingetupatia
gari ya wagonjwa?

Achana na
ambyulensi.
Tusingekosa
madawa!



Tumuangalie
mgonjwa
kwanza.

Hospitali ya Wilaya...

Subirini pemberi
kidogo, mpishe mtoto
wa mheshimiwa
kwanza.

MAPOKEZI







Tuna haki kuuliza.
Nataka kumwona
Mganga Mkuu.


MAPOKEZI

Usiku huu?
Kwanza wa
nini?


Tafadhalii ujibu
kwa adabu, sie
wazazi wako!
Ala.












Hapa si hospitali.
Mingesubiri. Au nendeni
vituo binafsi kama
mnataka express.

Huoni
huruma?

Acheni
ubishi.





Nilipata namba
yake kwenye
ubao wa hospitali.
Nampigia simu sasa
hivi. Usiondoke.

Haha...Mzee huo
utani. Katibu Mkuu,
akusikilizie tena usiku
huu? Wacha nikalale...

Nyumbani kwa Katibu Mkuu...






Shikamoo mzee! ...Ndiyo.
...Samahani sana, sikujua.
...Ndiyo, sasa hivi tu.
OK mzee.
...Haitatokea tena!



Samahani sana
ndugu zangu.
Unajua, aaah
inatokea. Nisubirini
nijiandae twende.


!!!?

Kesho yake.






Tunalipa kodi. Ni
haki yetu kikatiba.
Matibabu kwa wote
bila upendeleo.



Hospitali hii haipaswi
kukosa vifaa na
madawa ya dharura.



Wiki tatu baadae kijijini...

MAPOKEZ

Waaaah.! Afya
yako imerejea sasa!



Asante. Ajali yangu
itakuwa sadaka
kwa wengine.

MAPOKEZ

Unamaanisha
nini?




Babu Kibo alipotoa
taarifa kwa wakubwa,
nilihudumiwa kama
mfalme!

Nimeelewa! Mlipokua
hospitali, wacha
midawa imiminike
hana kituoni!

Kweli? Hebu
nichungulie
stoo!

HAPANA. Huko
huruhusiwi. Soma
ubaoni, nje.



Ila huo ujasiri wa kuvamia wakubwa mliutoa wapi?

Woga wa kutodai haki zetu unatuponza.

Mmetutia moyo.
Hatutawaangusha!

Nini kifanyike:

1. Haki zako zikivunjwa, mweleze kiongozi wa Serikali ya mtaa, washirikishe wanafamilia, marafiki na majirani.
2. Usijichukulie sheria mkononi, tafuta msaada wa sheria.
3. Kuwa tayari kutoa maoni yako na kuchukua hatua wakati wowote.
4. Uwe na uchachu wa mabadiliko katika jamii yako.

ZAHANATI

| URDHA YA DAWA ZILIZOPOZO:- | |
|----------------------------|----|
| 1. Tei-mu | Ba |
| 2. Seani Oan .. | 10 |
| 3. Fenegu | 5 |
| 4. Amfum- | 10 |
| 5. Dium | 0 |
| 6. Maguu | 9 |
| 7. Senton. | 45 |
| 8. Pem.. | 30 |
| 9. Mawenzi | 0 |
| Jumla | |
| | 69 |

